

Salamu kutoka NIKARAGUA!

Nikaragua ni nchi iliyoko Amerika ya Kati.
Takribani watu milioni 7 wanaishi huko!



KUENEZA INJILI

Wamisionari wa kwanza walikwenda Nikaragua mwaka 1953. Sasa kuna zaidi ya waumini 100,000 huko! Huko kuna hata hekalu lililo katika hatua za ujenzi.



PAPA WA ZIWA NIKARAGUA

Papa aina ya Bull wanaweza kuishi katika maji ya bahari *na* maji baridi. Hii inamaanisha wanaweza kuishi katika bahari, mito na maziwa. Wao wanaogelea kutoka Bahari ya Atlantiki kuitia mto mrefu na kuishi katika Ziwa la Nikaragua.

¿Nahki sma?

Hiyo inamaanisha
"Habari yako?"
katika Kimiskito!




VIELEO NA DAVE KLUG



PALO DE MAYO

Watu huko Nikaragua wanafanya sherehe kubwa ziitwazo Palo de Mayo majira ya mvua yanapokuja. Wanaupamba mtu au nguzo kwa riboni za rangi nydingi na kucheza kuuzunguka na kuwa na burudani ya mwezi mzima.




LUGHA

Lugha rasmi ni Kihispania. Baadhi ya watu pia huongea lugha za asili kama vile Kimiskito, Kisumu na Kirama.



Chuwis

Chuwis ni mchezo watoto wanaoucheza huko Nikaragua. Ili kuuchenza mchezo huu unahitaji maharage mabichi (au vijiti) na shimo ardhini (au kikombe). Toa maharage matano kwa kila mchezaji. Mchezaji wa kwanza anarusha harage bichi ndani ya shimo moja baada ya jingine. Kama anakosa moja, wanasimama, na mchezaji anayefuata anaendelea. Mchezaji wa kwanza kuingiza maharage mabichi yote matano shimonini anakuwa mshindi.



MAELEZO
YA UPISHI

Gallopinto

Huko Nikaragua, watu wengi wanakula mlo huu wa wali na maharage kila siku. Hapa kuna toleo unaloweza kujaribu!

1. Pasha **vijiko** **vya chakula** **2 vya mafuta** **na ½ ya kitunguu cha njano** **kilicho katwa katwa**. Koroga kwa dakika 5.
2. Koroga katika **vikombe** **1 ½ vya mchele mweupe** kwa dakika 2 hadi 3.
3. Ongeza **chumvi** **na vikombe** **3 vya maji**. Toa mbegu za **nusu ya pilipili hoho** na iweke juu yake.
4. Funika na upike kwa dakika 15 hadi maji yawe yanakaribia kuisha.
5. Tupa pilipili hoho iliyopikwa na koroga katika **vikombe** **2 vya maharage** **mekundu** **au meusi** **yaliyopikwa** **na ½ kijiko cha unga** **wa kitunguu swaamu**. Pika kwa dakika 10.

Hakikisha unapata msaada wa mtu mzima!